JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA UCHUKUZI

**MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI**

IMETHIBITISHWA ISO 9001

# TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

## MIFUMO YA TIKETI MTANDAO INAYOPEWA KIBALI CHA LATRA

***Dar es Salaam, Julai 02, 2025***

Kanuni za Tiketi Mtandao za Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini za mwaka 2024 zilizotangazwa katika Gazeti la Serikali Na. 20 la Januari 12, 2024 zimeweka takwa la mifumo ya tiketi mtandao nchini kupata kibali cha Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini. Kanuni ya 5 ya Kanuni hizo imeweka vigezo vya kupata kibali ambavyo ni pamoja na mfumo husika kuwa na ulinzi dhidi ya uvamizi wa kimtandao na kuwa na uwezo wa kuunganishwa na mifumo ya Serikali.

Mamlaka imeendelea kutoa elimu na kushirikiana na wadau husika ili kukamilisha matakwa ya Kisheria, kwa lengo la kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora za usafiri, kwa urahisi, zenye kuaminika na zenye ufanisi kwa wasafirishaji, watumia huduma na Serikali. Kazi hiyo hufanyika kwa ushirikiano wa wamiliki wa mifumo na wataalamu wa mifumo wa Serikali.

Hadi tarehe 30 Juni, 2025, kampuni tatu (3) za mifumo ya tiketi mtandao zimekidhi vigezo vya kupata kibali kwa mujibu wa Sheria, Mamlaka imeruhusu kampuni hizo kufanya malipo ya vibali na wakishafanya malipo hayo watakabidhiwa vibali vya kutoa huduma za tiketi mtandao. Mifumo hiyo ni

1. **Otapp Agency Company Limited**
2. **Hashtech Tanzania Limited na**
3. **Iyishe Company Limited**

Aidha, kampuni sita (6) za mifumo ya tiketi mtandao zimeonesha muelekeo mzuri, zinachangamoto ndogo ndogo, hivyo Mamlaka inatoa siku 14 kuanzia leo kuhakikisha wanakamilisha zoezi hilo, watakaoshindwa hawataruhusiwa kuendelea kutoa huduma ya tiketi mtandao, mifumo hiyo ni:

1. **AB Courier Express Limited**
2. **Busbora Company Limited**
3. **Logix Company Limited**
4. **Mkombozi Infotech Company**

5. **Sepatech Company Limited**
6. **Web Corporation Limited**

Kampuni mbili za mifumo ya tiketi mtandao zimebainika kuwa na changamoto kadhaa zinazowafanya kukosa sifa za msingi za kutoa huduma za tiketi mtandao. Hivyo wanapewa siku 7 za matazamio, wahakikishe wamekamilisha matakwa hayo, wakishindwa hawataruhusiwa kuendelea kutoa tiketi mtandao na wateja wao watashauriwa kuhamia kwa watoa huduma waliokamilisha utaratibu, mifumo hiyo ni:

1. **Duarani Innovative Company na**
2. **Itule Company**

Watoa huduma wote ambao hawapo katika orodha iliyotajwa hawatambuliki na Mamlaka kwa mujibu wa Sheria, hivyo Mamlaka inatoa rai kwa wasafirishaji kuwatumia watoa huduma za mauzo ya tiketi mtandao wanao tambulika ili kuepusha usumbufu unaoweza kujitokeza wakati wa ukaguzi utakaokuwa endelevu baada ya muda uliotolewa kuisha.

Kwa ujumla, watoa huduma wote wanapaswa kukamilisha na kuendelea kutekeleza matakwa ya kisheria ya kuunganisha mifumo yao na mfumo mkuu wa tiketi mtandao (CeTS) ikiwa ni pamoja na kuingiza taarifa za mabasi yote wanayoyahudumia kwenye mfumo jumuishi wa tiketi mtandao wa Mamlaka (UTS). Wataalamu wetu wataendelea kufanya ukaguzi endelevu na hatua za Kisheria zitachukukuliwa kwa watoa huduma watakaobainika kukiuka.

Pia, Mamlaka inawakumbusha wadau wote kuwa mfumo jumuishi wa tiketi mtandao umesanifiwa kuwawezesha watumiaji wote wa huduma za **usafiri wa treni za Reli ya Kisasa (SGR), Reli ya Kati (MGR) na mabasi yaendayo mikoani na nchi jirani** kukata tiketi wenyewe popote walipo. Mfumo huo unapatikana kupitia simu janja au kompyuta kwa anwani ya **tiketi.latra.go.tz** wadau wote mnakaribishwa kutumia mfumo huo.

Mamlaka inatoa shukrani za dhati kwa wasafirishaji, Shirika la Reli Nchini (TRC), Chama cha Wamiliki wa Mabasi (TABOA), wamiliki wa mifumo ya tiketi mtandao na wadau wengine kwa ushirikiano wao katika kutekeleza kanuni za tiketi mtandao na kuboresha huduma za usafiri nchini.

Digitally Signed By Salum PAZZY
Wed Jul 02 16:14:05 EAT 2025

Salum PAZZY
**Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano**